JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA
**BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA**

# TAARIFA YA UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WATAHINIWA KATIKA MTIHANI WA UALIMU CHETI DARAJA LA A (GATCE) 2020

636 TEHAMA

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA

BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA

# TAARIFA YA UCHAMBUZI WA MAJIBU KATIKA MTIHANI WA UALIMU DARAJA LA A

# (GATCE) 2020

# 636 TEHAMA

*Imechapishwa na:*
Baraza la Mitihani laTanzania,
S.L.P 2624,
Dar es Salaam,Tanzania.

**©Baraza la Mitihani la Tanzania, 2020**

Haki zote zimehifadhiwa.

# YALIYOMO


DIBAJI ..... iv
1.0 UTANGULIZI ..... 1
2.0 TATHMINI YA MAJIBU YA WATAHINIWA KWA KILA SWALI ..... 2
2.1 SEHEMU A ..... 2
2.1.1 Swali la 1: Misingi ya Ufundishaji na Ujifunzaji wa Somo la TEHAMA ..... 2
2.1.2 Swali la 2: Upimaji ..... 5
2.1.3 Swali la 3: Ufundishaji wa Mada za Mfano ..... 8
2.1.4 Swali la 4: Upimaji ..... 10
2.1.5 Swali la 5: Ufundishaji wa Mada za Mfano ..... 11
2.1.6 Swali la 6: Maandalizi ya Ufundishaji na Ujifunzaji wa Somo la TEHAMA ..... 14
2.1.7 Swali la 7: Maandalizi ya Ufundishaji na Ujifunzaji wa Somo la TEHAMA ..... 16
2.1.8 Swali la 8: Ufundishaji wa Mada za Mfano ..... 18
2.1.9 Swali la 9: Ufundishaji wa Mada za Mfano ..... 20
2.1.10 Swali la 10: Ufundishaji wa Mada za Mfano ..... 22
2.2 SEHEMU B ..... 24
2.2.1 Swali la 11: Misingi ya Ufundishaji na Ujifunzaji wa Somo la TEHAMA ..... 25
2.2.2 Swali la 12: Ufundishaji wa Mada za Mfano ..... 28
2.2.3 Swali la 13: Upimaji ..... 32
2.2.4 Swali la 14: Misingi ya Ufundishaji na Ujifunzaji wa Somo la TEHAMA ..... 36
2.2.5 Swali la 15: Ufundishaji wa Mada za Mfano ..... 39
2.2.6 Swali la 16: Ufundishaji wa Mada za Mfano ..... 42
3.0 UCHAMBUZI WA KIWANGO CHA UFAULU KATIKA MADA ..... 44
4.0 HITIMISHO ..... 45
5.0 MAPENDEKEZO ..... 45
*Kiambatisho* ..... 46

**DIBAJI**

Baraza la Mitihani la Tanzania limeandaa taarifa juu ya uchambuzi wa majibu ya watahiniwa wa somo la TEHAMA 2020. Taarifa hii imeandaliwa kwa lengo la kutoa mrejesho kwa wadau wa elimu, wanachuo, wakufunzi na watunga sera jinsi ambavyo watahiniwa walijibu maswali ya mtihani. Majibu ya watahiniwa ni kiashiria kimojawapo kinachoonesha maarifa na stadi ambazo waliweza au walishindwa kupata katika kipindi cha miaka miwili ya masomo yao.

Taarifa hii ni tathmini inayoonesha mambo ambayo yalisababisha watahiniwa kushindwa kujibu maswali kwa usahihi. Sababu hizo ni pamoja na kutoelewa matakwa ya maswali au kutokuwa na maarifa ya kutosha katika mada walizopimwa. Aidha, uchambuzi unaonesha kuwa, watahiniwa waliokuwa na kiwango kizuri cha ufaulu walikuwa na maarifa ya kutosha katika mada zilizopimwa, kwa hiyo waliweza kujibu maswali kwa ufasaha. Uchambuzi umefanyika kwa kila swali kuonesha idadi na asilimia ya watahiniwa waliokuwa na kiwango kizuri cha ufaulu, wastani na hafifu. Vilevile, uchambuzi huu unaonesha uwezo na udhaifu wa watahiniwa katika kujibu maswali. Aidha, uchambuzi wa kiwango cha ufaulu kwa kila mada husika umefanyika.

Mwisho, Baraza la Mitihani linapenda kuwashukuru maafisa mitihani, wakufunzi wa somo na wadau wote walioshiriki katika uchambuzi wa takwimu na kuandaa taarifa hii.



Dkt Charles E. Msonde
**KATIBU MTENDAJI**

## 1.0 UTANGULIZI

Taarifa hii imeandaliwa kutokana na uchambuzi wa majibu ya watahiniwa wa somo la TEHAMA kwa Mtihani wa Ualimu Daraja la A uliofanyika Juni 2020. Mtihani huu ulitungwa kwa kuzingatia Muhtasari wa somo la TEHAMA wa mwaka 2009 na ulikuwa na maswali 16 ambayo yaligawanyika katika sehemu mbili: A na B. Sehemu A ilikuwa na maswali 10 ya lazima yaliyohitaji majibu mafupi. Kila swali lilikuwa na alama 4. Sehemu B ilikuwa na maswali 6 ya insha ambapo mtahiniwa alitakiwa kujibu maswali manne. Katika sehemu hii kila swali lilikuwa na alama 15. Mtihani huu ulikuwa na jumla ya alama 100 ambapo sehemu A ilikuwa na alama 40 na sehemu B alama 60.

Jumla ya watahiniwa 3,698 walifanya mtihani huu, kati yao watahiniwa 3,520 ni watahiniwa wa kawaida (GATCE) na watahiniwa 178 walifanya mtihani maalum (GATSCCE). Kiwango cha ufaulu cha watahiniwa katika somo la TEHAMA kwa mwaka 2020 kilikuwa ni kizuri kwani watahiniwa 3,697 (99.9%) walifaulu kwa kupata wastani wa alama 40 au zaidi. Viwango vya ufaulu vimegawanyika katika makundi matatu ambayo ni: kizuri, wastani na hafifu. Kiwango kizuri ni kuanzia asilimia 70 hadi 100; kiwango cha wastani asilimia 40 hadi 69 na kiwango hafifu ni asilimia 0 hadi 39 ya jumla ya alama katika swali husika. Aidha, chati na majedwali vimeambatishwa ili kufafanua ufupisho wa takwimu za ufaulu kwa watahiniwa. Katika ufupisho huo rangi ya kijani inawakilisha ufaulu kwa kiwango kizuri, rangi ya njano inawakilisha kiwango cha wastani na kiwango hafifu kinawakilishwa na rangi nyekundu.

Katika taarifa hii maswali yaliyojibiwa vizuri, wastani na hafifu yamechambuliwa ili kuboresha zaidi ufundishaji na ujifunzaji wa somo la TEHAMA. Uchambuzi huu unaonesha matakwa ya swali, jinsi watahiniwa walivyojibu maswali na makosa waliyofanya wakati wa kujibu maswali husika. Vilevile, baadhi ya vielelezo vya majibu sahihi na majibu yasiyo sahihi vimeambatanishwa kwa ufafanuzi zaidi. Maoni na hitimisho limetolewa mwishoni mwa taarifa hii.


## 2.0 TATHMINI YA MAJIBU YA WATAHINIWA KWA KILA SWALI

### 2.1 SEHEMU A

Sehemu A ya mtihani huu ina maswali ya majibu mafupi 10 ambapo watahiniwa walitakiwa kujibu maswali yote. Kila swali lilikuwa na alama nne hivyo kufanya jumla ya alama 40 katika sehemu hii. Kiwango cha ufaulu katika kila swali kiligawanyika katika sehemu kuu tatu ambazo ni alama 0 hadi 1.5 kiwango hafifu, alama 2 hadi 2.5 kiwango cha wastani na alama 3 hadi 4 kiwango kizuri.

#### 2.1.1 Swali la 1: Misingi ya Ufundishaji na Ujifunzaji wa Somo la TEHAMA

Swali hili lilimtaka mtahiniwa kubainisha mbinu nne anazoweza kutumia mwalimu wa somo la TEHAMA kufundisha msingi wa ufundishaji unaoweka usawa wa kijinsia darasani. Uchambuzi wa takwimu unaonesha kuwa, watahiniwa 3,698 sawa na asilimia 100 walifanya swali hili. Kati yao, watahiniwa 1,286 (34.8%) walipata alama kuanzia 3 hadi 4, watahiniwa 1,734 (46.9%) walipata alama kuanzia 2 hadi 2.5. Aidha, takwimu zinaonesha kuwa watahiniwa 678 (18.3%) walikuwa na kiwango hafifu cha ufaulu na walipata alama kuanzia 0 hadi 1.5. Chati Na. 1 inaonesha ufupisho wa takwimu katika swali hili.





**Chati Na. 1:** *Kiwango cha ufaulu cha watahiniwa katika swali la 1.*

Kwa ujumla, watahiniwa katika swali hili walifaulu kwa kiwango kizuri kwani watahiniwa 3,020 (81.7%) walipata alama kuanzia 2 hadi 4.

Hata hivyo, pamoja na swali hili kuwa na kiwango kizuri cha ufaulu baadhi ya watahiniwa 1,734 (46.9%) walifaulu kwa kiwango cha wastani. Hawa walitoa hoja mbili sahihi zinazobainisha mbinu za kufundishia msingi wa ufundishaji na unaoweka usawa wa kijinsia darasani na kutoa hoja nyingine mbili ambazo si sahihi kulingana na matakwa ya swali. Uchambuzi zaidi ulionyesha kuwa, watahiniwa hawa walichanganya njia za kufundishia ambazo zinazingatia na zile zisizozingatia usawa wa jinsia. Kwa mfano baadhi ya watahiniwa waliandika mbinu kama vile: *mhadhara na maonesho.* Watahiniwa walitakiwa kujua kwamba mhadhara na maonesho hazizingatii usawa wa kijinsia kwa sababu zinahusisha mtu mmoja mmoja tu.

Asilimia 34.8 ya watahiniwa walifaulu kwa kiwango kizuri kwa kupata alama 3 hadi 4. Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa ulionesha kuwa, watahiniwa hawa walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu mbinu za kufundishia msingi wa ufundishaji unaoweka usawa wa kijinsia darasani, jambo ambalo liliwawezesha kujibu swali kwa ufasaha. Watahiniwa walibainisha mbinu sahihi mbalimbali kama vile: *Majadiliano katika* makundi, *maswali na majibu, maigizo na nyimbo*. Aidha, baadhi yao hawakupata alama zote kwa sababu walibainisha mbinu kwa kuzirudia rudia. Kwa mfano, baadhi ya watahiniwa walibainisha mbinu ya "majadiliano katika vikundi" na "changanya kete" kama mbinu mbili tofauti badala ya mbinu moja. Kielelezo Na. 1.1 kinaonesha sampuli ya jibu sahihi kutoka kwa mmoja wa watahiniwa.



1: 1. Majadiliano katika vikundi ambapo kuna kuwa na mchanganyiko wa jinsia kati ya mwanafunzi mvulana na msichana kwa idadi sawa.

2. Maswali na majibu, kwa kuuliza maswali mbalimbali ambayo huhitaji kujibu wanafunzi wote.


3. Igizo dhima ambapo kutakuwa na mchanganyiko wa wahusika wa jinsia zote

4. Nyimbo ambapo atahusisha jinsia zote za wanafunzi katika uimbaji huo.

Kielelezo Na. 1.1: Sampuli ya jibu sahihi katika swali la 1.

Kielelezo Na. 1.1 kinaonesha majibu ya mtahiniwa ambaye alibainisha kwa usahihi mbinu anazoweza kutumia mwalimu wa somo la TEHAMA kufundisha msingi wa ufundishaji unaoweka usawa wa kijinsia.

Uchambuzi ulionesha pia kwamba, watahiniwa 678 (18.3%) walifaulu kwa kiwango hafifu katika swali hili. Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa ulionesha kuwa, watahiniwa walibainisha viashiria vya ufundishaji usioweka usawa wa kijinsia darasani. Uchambuzi zaidi ulionesha kuwa, baadhi yao walibainisha mbinu za kutambua ufundishaji usioweka usawa darasani. Kwa mfano, baadhi ya watahiniwa waliandika: *kutoa fursa sawa kwa wanafunzi, kutoonesha upendeleo baina ya wanafunzi, kuwashirikisha wanafunzi wote katika vitendo mbalimbali, kuadhibu wanafunzi wenye kufanya unyanyasaji wa kijinsia dhidi ya jinsia nyingine*. Majibu haya yanaonesha kuwa, watahiniwa walishindwa kubainisha mbinu husika kwenye maelezo yao. Kielelezo Na. 1.2 kinaonesha sampuli ya jibu la mmoja wa watahiniwa walioshindwa kubainisha mbinu sahihi.



1. (i) Kutoa madaraka. Mwalimu anatakiwa kuchanganya jinsia zote wavulana na wasichana katika kuwapa nafasi ya uongozi.
(ii) Mkao darasani - Katika kila upande darasani Mwalimu unatakiwa uwaweke jinsia zote na si upande mmoja tu. ili wasije ona kua wengine wanapendelewa.
(iii) Kutoa motisho darasani. ili mwalimu aweze kuzingatia usawa wa kijinsia darasani anapouliza swali anatakiwa kutoa motisha kwa wanafunzi wote darasani.
(v) Kuchagua jinsia zote katika kujibu maswali. Kuna walimu wengine wanatabia ya kubagua wanafunzi kutokana na uwezo, jinsia zao hivyo katika ufundishaji unapouliza swali unatakiwa kuwashirikisha wote katika kujibu.

Kielelezo Na. 1.2: Sampuli ya jibu ambalo siyo sahihi katika swali la 1.

Kielelezo Na. 1.2 kinaonesha majibu ya mmoja wa watahiniwa ambaye alibainisha mbinu anazoweza kuzitumia ili kuweka usawa wa kijinsia darasani badala ya mbinu anazoweza kutumia mwalimu wa somo la TEHAMA kufundishia msingi wa ufundishaji unaoweka usawa wa kijinsia darasani.

### 2.1.2 Swali la 2: Upimaji

Swali hili lililenga kupima ufahamu wa watahiniwa kuhusu mkoba wa kazi. Mtahiniwa alitakiwa kuainisha faida nne za mkoba wa kazi kama zana ya upimaji wa maendeleo ya mwanafunzi. Jumla ya watahiniwa 3,698 (100%) walifanya swali hili. Kati ya hao watahiniwa 803 (21.7%) walipata alama kuanzia 3 hadi 4. Watahiniwa 1,468 (39.7%) walipata alama kuanzia 2 hadi 2.5 na watahiniwa 1,427 (38.6%) walipata alama 0 hadi 1.5. Takwimu hizi zinadhihirisha kuwa, watahiniwa walifaulu katika kiwango cha wastani katika swali hili kama inavyooneshwa katika Jedwali Na. 1.

**Jedwali Na.1: Ufaulu wa Watahiniwa Katika Swali la 2**

| Alama | Idadi ya Watahaniwa | Asilimia ya Watahiniwa |
|---|---|---|
| 0 - 1.5 | 1,427 | 38.6 |
| 2.0 - 2.5 | 1,468 | 39.7 |
| 3.0 - 4.0 | 803 | 21.7 |

Kwa ujumla swali hili lilikuwa na kiwango cha ufaulu cha wastani kwani asilimia 61.4 ya watahiniwa walipata alama kuanzia 2 hadi 4. Katika swali hili watahiniwa 1,468 sawa na asilimia 39.7 walifaulu kwa kiwango cha wastani kama ilivyooneshwa kwenye Jedwali Na.1. Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa ulionyesha kuwa, wengi wao walielewa faida za mkoba wa kazi kwa ujumla lakini walichanganya na faida za kufanya tathmini kwa mwanafunzi. Kwa mfano, baadhi ya watahainiwa waliandika: *humsaidia mwalimu kuboresha mbinu za ufundishaji, humsaidia mwalimu kubaini maeneo ambayo mwanafunzi hakuelewa.* Aidha, baadhi ya watahiniwa waliainisha kwa usahihi faida mbili tu kati ya nne zilizotakiwa. Faida zilizoainishwa na watahiniwa wengi ni: *humsaidia mwanafunzi kutunza kumbukumbu na humsaidia mwanafunzi kujikumbushia mambo aliyojifunza*. Hii huenda imetokana na watahiniwa wenyewe kutumia mikoba ya kazi, hivyo kuwafanya kukumbuka faida hizo kwa urahisi.

Kwa upande mwingine, baadhi ya watahiniwa 1,427 (38.6%) waliofaulu kwa kiwango hafifu kwa kupata alama kuanzia 0 hadi 1.5 waliainisha faida za kutumia njia ya utafiti katika kufundisha. Kwa mfano baadhi ya watahiniwa walianisha faida kama: *huwapa wanafunzi uwezo wa kutafuta taarifa za somo, huwafanya wanafunzi watumie muda wa ziada vizuri, hukuza stadi ya kujiamini na hukuza ushirikiano baina ya wanafunzi.* Watahiniwa wengine waliainisha faida za kutumia ufundishaji kwa vitendo badala ya faida za mkoba wa kazi. Uchambuzi zaidi ulibaini kuwa, baadhi ya watahiniwa waliandika faida za andalio la somo kwa mwalimu wakati wengine walieleza faida za mwalimu kuwa na mkoba wa kuhifadhia vifaa vya kufundishia. Hii inadhihirisha kuwa, watahiniwa walikuwa hawana uelewa halisi wa maana na madhumuni ya mkoba wa kazi. Kielelezo Na. 2.1 kinaonesha sampuli ya jibu ambalo siyo sahihi.

2\. i/ Husaidia kuonyesha uwezo wa mwanafunzi katika kubuni, kudadisi na kuchunguza mambo mbalimbali.
ii/ Humjengea kumbukumbu ya kudumu.
iii/ Humfanya mwanafunzi ashiriki kikamilifu katika shughuli za ufundishaji na ujifunzaji.
iv/ Humfanya mwanafunzi ajenge dhana halisi juu ya kile anachochunguza.

Kielelezo Na. 2.1: Sampuli ya jibu ambalo siyo sahihi katika swali la 2.

Kielelezo Na. 2.1 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyeeleza faida za kutumia vitendo katika ufundishaji badala ya faida za mkoba wa kazi.

Asilimia 21.7 ya watahiniwa waliopata alama kuanzia 3 hadi 4 walikuwa na uelewa mzuri katika mada ya upimaji. Watahiniwa hao waliweza kuainisha kwa usahihi faida za mkoba wa kazi. Hata hivyo baadhi yao hawakupata alama zote 4 kutokana na kutokutoa maelezo yanayojisholeza. Kielelezo Na. 2.2 kinaonesha sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyejibu kwa usahihi.


2 Faida (au) za mkoba wa kazi kama zana ya Upimaji wa maendeleo ya mwanafunzi ni:
i) kubaini changamoto ya Ujifunzaji kwa mwanafunzi, Mfano kutoelewa mada fulani.
ii) kutambua maendeleo ya mwanafunzi kitaaluma, Mfano alama za mitihani anazopata.
iii) kutunza kumbu kumbu, Mfano mitihani, majaribio.
iv) Husaidia wanafunzi kujisomea kwa muda wa ziada, Mfano uwepo wa mitihani, Majaribio, hufanya waweze kujisomea.

Kielelezo Na. 2.2: Sampuli ya jibu sahihi katika swali la 2.

Kielelezo Na. 2.2 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyeeleza faida za mkoba wa kazi kwa usahihi.

### 2.1.3 Swali la 3: Ufundishaji wa Mada za Mfano


Swali hili lilitoka katika mada ya *Ufundishaji wa Mada za Mfano* na lilimtaka mtahiniwa kufafanua kwa kifupi aina ya huduma zinazotolewa na UMATI, EMAU, ANGAZA na AMREF – TANZANIA. Watahiniwa 3,698 (100%) walifanya swali hili, kati yao watahiniwa 747 (20.2%) walipata alama kuanzia 3 hadi 4. Watahiniwa 271 (7.3%) walipata alama kuanzia 2 hadi 2.5 na watahiniwa 2,680 (72.5%) walipata alama kuanzia 0 hadi 1.5. Chati Na. 2 inaonesha ufaulu kwa watahiniwa katika swali hili.




**Chati Na. 2:** *Ufaulu kwa watahiniwa kwa asilimia katika swali la 3.*

Kwa ujumla kiwango cha ufaulu cha watahiniwa katika swali hili kilikuwa hafifu kwa sababu asilimia 72.5 ya watahiniwa walipata alama chini ya 2. Kati yao asilimia 56.1 ya watahiniwa walipata alama sifuri. Uchambuzi uliofanyika katika majibu ya watahiniwa ulibaini kuwa watahiniwa wengi walikuwa hawana ufahamu juu ya huduma zinazotolewa na mashirika ya UMATI, EMAU, ANGAZA na AMREF katika jamii kwani baadhi yao waliandika majibu yanayojumuisha mashirika yote badala ya kuandika huduma inayotolewa kwa kila shirika. Kwa mfano baadhi ya watahiniwa waliandika: *huduma amabazo hutolewa na UMATI, EMAU, ANGAZA na AMREF ni kutoa misaada ya chakula, nguo na malazi kwa familia zilizokumbwa na majanga kama mafuriko au moto*.

Uchambuzi ulionyesha pia kuwa, baadhi yao waliandika majina ya mashirika tu bila kuandika maelezo yoyote. Hata hivyo, watahiniwa wachache walitoa maelezo sahihi juu ya shirika moja tu la ANGAZA hii ni kwa sababu shirika hili linatoa huduma zake kwenye vituo vya zahanati na hospitali na hutoa matangazo ya huduma zake kwenye vyombo vya habari kama vile luninga, majarida na redio. Kielelezo Na. 3 kinaonesha sampuli ya jibu ambalo siyo sahihi kutoka kwa mmoja wa watahiniwa.


3. Kufafanua Kwa kifupi aina ya huduma zinazotolewa na -
UMATI - hutoa huduma za usafiri wa majini,
EMAU - hutoa elimu Masafa Ulimwenguni,
ANGAZA - hutoa huduma za usafiri wa angani,
AMREF - TANZANIA - husimamia wakimbizi Tanzania

Kielelezo Na. 3: Sampuli ya jibu la swali la 3 ambalo siyo sahihi.


Kielelezo Na. 3 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyetafsiri kimakosa vifupisho vya kila shirika kutokana na kukosa uelewa wa kutosha juu ya huduma zinazotolewa na mashirika ya UMATI, EMAU, ANGAZA na AMREF.

Pamoja na swali kuwa na ufaulu hafifu, watahiniwa 747 (20.2%) walikuwa na kiwango kizuri cha ufaulu kwa kupata alama 3 hadi 4. Watahiniwa hawa walikuwa na uelewa mzuri kuhusu aina ya huduma zinazotolewa na UMATI, EMAU, ANGAZA na AMREF – TANZANIA. Majibu yaliyotolewa na watahiniwa ni pamoja na "*UMATI – ni kituo kinachoshughulika na kutoa maelekezo sahihi ya uzazi wa mpango pamoja na malezi bora kwa mtoto, EMAU – hutoa elimu inayohusiana na malezi ya vijana katika maisha yao, ANGAZA – ni kituo ambacho huto a elimu inayohusiana na njia na namna ya kujikinga na maambukizi ya ugonjwa wa UKIMWI, AMREF – TANZANIA – hiki ni kituo kinachohusika na utafiti wa magonjwa mbalimbali nchini Tanzania ambayo hutafutiwa uchunguzi ili kuweza kupata dawa yake*". Hata hivyo, baadhi yao hawakupata alama zote kwa sababu walishindwa kufafanua aina ya huduma inayotolewa na UMATI. Hii ni kwa sababu shirika hili kwa sasa halina ofisi zake katika hospitali mbalimbali.

### 2.1.4 Swali la 4: Upimaji


Swali hili lililenga kupima ufahamu wa watahiniwa kuhusu faida mbili na kasoro mbili za mwalimu kutumia maswali ya "kweli" na "si kweli" katika mazoezi na mitihani kwa wanafunzi wake.

Watahiniwa 3,698 (100%) walifanya swali hili, kati yao watahiniwa 3,493 (94.5%) walipata alama kuanzia 3 hadi 4 na watahiniwa 179 (4.8%) walipata alama kuanzia 2 hadi 2.5. Uchambuzi wa takwimu unaonesha kuwa watahiniwa 26 (0.7%) walipata alama kuanzia 0 hadi 1.5. Chati Na. 3 inaonesha ufaulu kwa watahiniwa katika swali hili.




**Chati Na. 3:** *Ufaulu kwa watahiniwa kwa asilimia katika swali la 4.*

Kwa ujumla kiwango cha ufaulu cha watahiniwa katika swali kilikuwa kizuri kwa sababu asilimia 99.3 ya watahiniwa walipata alama zaidi ya 1.5 kama inavyoonekana kwenye Chati Na. 3. Kiwango hiki kizuri cha ufaulu kinaonesha kuwa watahiniwa walikuwa na uelewa wa kutosha kuhusu faida na kasoro za matumizi ya maswali ya "kweli na si kweli" katika mazoezi na mitihani. Watahiniwa hao walijibu kwa kuonesha faida na kasoro tatu hadi nne za mwalimu kutumia maswali ya "kweli na si kweli" katika mazoezi na mitihani. Faida zilizoelezwa na baadhi ya watahiniwa ni pamoja na *maswali hayo ni rahisi kutunga na huweza kupima sehemu kubwa ya maudhui*. Vilevile kasoro ya *kubuni majibu ilielezwa na watahiniwa wengi*. Kielelezo Na. 4 ni sampuli ya majibu ya mmoja wa watahiniwa waliojibu swali hili kwa usahihi.



4. Faida
- Kuokoa muda wakati wa usahihishaji hivyo ni rahisi kuyasahihisha.
- Ni rahisi kuyatunga.

Hasara.
- Mwanafunzi anaweza kuotea jibu kama halijui na akalipata.
- Ni rahisi kuibia.

Kielelezo Na. 4**:** Sampuli ya jibu sahihi katika swali la 4.


Kielelezo Na. 4 ni jibu la mtahiniwa aliyeonesha kwa usahihi faida na kasoro za maswali ya kweli na si kweli.

Pamoja na watahiniwa wengi kuwa na kiwango kizuri cha ufaulu, asilimia 4.8 ya watahiniwa walikuwa na kiwango cha wastani na asilimia 0.7 walikuwa na kiwango hafifu cha ufaulu. Uchambuzi unaonesha kuwa baadhi yao walionesha faida za maswali ya kweli au si kweli kwa usahihi lakini walichanganya kasoro za maswali ya kweli au si kweli na zile za maswali ya kuchagua. Wengine walichanganya faida za maswali ya kuchagua na zile za maswali ya kweli au si kweli. Kwa mfano, baadhi ya watahiniwa waliandika: *Maswali ya kweli au si kweli ni magumu kutunga* kama kasoro ya maswali ya kweli au si kweli. Watahiniwa hawa hawakuwa sahihi kwa sababu maswali ya kuchagua ndiyo magumu kutunga yakilinganishwa na maswali ya kweli au si kweli. Uchambuzi zaidi ulibaini kuwa, watahiniwa wachache waliopata kiwango hafifu cha ufaulu walieleza faida na kasoro za kutumia nyanja za juu katika kufanya tathmini. Kwa mfano, baadhi ya watahiniwa waliandika: *humuwezesha mwanafuzi kufikiri zaidi na humuwezesha mwanafunzi kutokubuni majibu*. Majibu haya ya watahiniwa yanadhihirisha kuwa, hawakuelewa matakwa ya swali.

### 2.1.5 Swali la 5: Ufundishaji wa Mada za Mfano


Swali hili lililenga kumpima mtahiniwa juu ya uelewa wa kutumia mawasiliano kwa njia ya barua pepe. Katika swali hili mtahiniwa alitakiwa kutoa hoja za kutetea kuwa mawasiliano kwa njia ya barua pepe ni bora kuliko barua za kawaida ambapo mtahiniwa alitakiwa kutoa hoja nne.

Watahiniwa wote 3,698 (100%) walifanya swali hili, kati yao watahiniwa 3,632 (98.2%) walipata alama kuanzia 3 hadi 4. Watahiniwa 34 (0.9%) walipata alama kuanzia 2 hadi 2.5 na watahiniwa 32 (0.9%) walipata alama 0 hadi 1.5. Kwa ujumla swali hili lilikuwa na kiwango kizuri cha ufaulu kwa sababu asilimia 99.1 ya watahiniwa walipata alama zaidi ya 2 kama inavyooneshwa katika Chati Na. 4.




**Chati Na. 4:** *Ufaulu kwa watahiniwa katika swali la 5.*

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa katika swali hili unaonesha kuwa, asilimia 98.2 ya watahiniwa waliofaulu kwa kiwango kizuri kwa kupata alama kuanzia 3 hadi 4 walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu ubora wa njia ya mawasiliano kwa kutumia barua pepe kuliko barua ya kawaida. Kiwango hiki kizuri cha ufaulu huenda kimesababishwa na watu wengi kwenye jamii kutumia intaneti na barua pepe kufanya mawasiliano binafsi na ya kibiashara. Hoja zilizotolewa na watahiniwa wengi ni pamoja na: *Ufikishwaji wa ujumbe kwa haraka, barua pepe hutumia gharama ndogo katika usafirishaji wake, usalama wa barua pepe ni wa uhakika ikilinganishwa na barua za kawaida*. Hata hivyo, baadhi ya watahiniwa hawakupata alama zote kwa sababu walitoa maelezo yasiyojisholeza kwani maelezo yao yalieleza upande wa barua pepe bila kueleza barua za kawaida. Kielelezo Na. 5 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu swali kwa usahihi.



5. (a) Usafirishaji wa ujumbe kwa haraka, kutokana barua pepe kutuma ujumbe kwa kutumia intaneti au mtandao mengine ya kielectroniki hupelekwa ujumbe kupitia kwa haraka kwa mtu aliyekusudiwa kupokea tofauti na barua za kawaida mpaka iende posta au mtu apeleke kwa miguu.

(b) Gharama ndogo, barua pepe hutumia gharama ndogo katika usafirishaji wake na uandaaji wake tofauti na barua za kawaida hutumia gharama kubwa kama vile kubandika stempu na kulipia usafirishaji wake.

(c) Hutumia muda mchache katika kuandaa, kutokana barua pepe kuwa na sehemu tatu tu ambazo ni kichwa cha barua, kiini na mengine kumesababisha kutumia mchache kuandaa barua hiyo tofauti na barua ya kawaida kutumia vipengele vingi kama vile anuani ya mwandishi na mwandikiwa, kichwa cha barua, kiini na hitimisho.

(d) Usalama, barua pepe huweza kusafirishwa na kupitia kwa usalama zaidi kutokana na kutumia mtandao wa intaneti tofauti na barua za kawaida ambazo huweza kusafirisha mtu kwa miguu ambaye anaweza kubadili taarifa za awali au kupoteza barua husika

Kielelezo Na. 5: Sampuli ya jibu sahihi katika swali la 5.

Kielelezo Na. 5 ni jibu la mtahiniwa aliyetoa hoja zenye mantiki zinazotetea matumizi ya mawasiliano kwa njia ya barua pepe kuwa ni bora kuliko barua za kawaida.

Watahiniwa (0.9%) waliofaulu kwa kiwango cha wastani waliweza kutoa hoja mbili kati ya nne zilizotakiwa katika swali hili. Baadhi ya watahiniwa waliorodhesha hoja zote kwa usahihi lakini hawakutoa maelezo yoyote. Aidha, watahiniwa waliokuwa na kiwango hafifu cha ufaulu hawakuelewa matakwa ya swali kwani wengi wao waliandika changamoto zinazotokana na matumizi ya barua pepe. Kwa mfano baadhi yao waliandika: *Barua pepe hutumiwa na watu wenye ujuzi wa kutumia kompyuta au simu, vilevile barua pepe hutumia gharama kubwa kuweza kupata vifaa vinavyoweza kufanya mawasiliano ya intaneti.*

### 2.1.6 Swali la 6: Maandalizi ya Ufundishaji na Ujifunzaji wa Somo la TEHAMA


Swali hili lililenga kupima maarifa ya watahiniwa katika kuchambua muhtasari wa somo la TEHAMA. Watahiniwa walitakiwa kubainisha mambo manne anayopaswa kufanya mwalimu wa somo la TEHAMA wakati wa kuchambua muhtasari wa somo. Watahiniwa waliofanya swali hili walikuwa 3,698 sawa na asilimia 100. Kati yao watahiniwa 2,302 (62.2%) walipata alama kuanzia 3 hadi 4 na watahiniwa 476 (12.9%) walipata alama kuanzia 2 hadi 2.5. Uchambuzi wa takwimu unaonesha kuwa watahiniwa 920 sawa na asilimia 24.9 walipata alama 0 hadi 1.5. Kwa ujumla, kiwango cha ufaulu cha watahiniwa katika swali hili ni kizuri kwa sababu asilimia 75.1 ya watahiniwa walipata alama zaidi ya 1.5 kama inavyooneshwa katika Jedwali Na. 2.

**Jedwali Na.2: Ufaulu wa Watahiniwa Katika Swali la 6**

| Alama | Idadi ya Watahaniwa | Asilimia ya Watahiniwa |
|---|---|---|
| 0 - 1.5 | 920 | 24.9 |
| 2.0 - 2.5 | 476 | 12.9 |
| 3.0 - 4.0 | 2,302 | 62.2 |

Watahiniwa (47.7%) waliweza kubainisha kwa usahihi mambo manne anayopaswa kufanya mwalimu wa somo la TEHAMA wakati wa kuchambua muhtasari wa somo. Baadhi ya mambo waliyobainisha ni: *kubaini mada zilizopo kwenye muhtasari, kubaini mbinu zinazopaswa kufundishia mada husika na malengo ya somo.* Majibu hayo ya watahiniwa yalionesha kuwa walikuwa na maarifa ya kutosha katika mambo wanayopaswa kuzingatia wakati wa kuchambua muhtasari wa somo. Hata hivyo, baadhi ya watahiniwa walishindwa kupata alama zote kwa sababu

walibainisha mambo yanayopaswa kufanywa na mwalimu wa somo la TEHAMA wakati wa kuchambua muhtasari kwa kuchanganya na mambo anayopaswa kufanya mwalimu wakati wa kuandaa azimio la kazi. Kwa mfano baadhi ya watahiniwa walibainisha kuwa *mwalimu huangalia kalenda ya shule na kalenda ya mwaka* wakati wa kuandaa azimio la kazi. Kielelezo Na. 6.1 ni sampuli ya mtahiniwa aliyeweza kujibu swali hili kwa usahihi.



06. i. Abainishe malengo ya kila mada
ii. Abainishe mbinu zinazopaswa kufundishi a mada husika
iii. Ajue zana atakazotumia kufundishia mada husika
iv. Abainishe vipindi atakavyotumia kufu ndishia mada husika.

Kielelezo Na. 6.1: Sampuli ya jibu sahihi katika swali la 6.

Kielelezo Na. 6.1 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyebainisha kwa usahihi mambo anayopaswa kuzingatia mwalimu wa somo la TEHAMA wakati wa kuchambua muhtasari wa somo.

Aidha, watahiniwa 920 (24.9%) waliopata kiwango hafifu cha ufaulu walibainisha mambo anayopaswa kufanya mwalimu wakati wa kuandaa andalio la somo. Kwa mfano baadhi ya watahiniwa waliandika: *mwalimu anatakiwa kuwa na kitabu cha kiada, kiongozi cha mwalimu na zana za kufundishia*. Wengine walibainisha mambo anayopaswa kufanya mwalimu wakati wa kuandaa azimio la kazi. Majibu haya ya watahiniwa yanadhihirisha kuwa walishindwa kutofautisha mambo ya kuzingatia wakati wa kuchambua muhtasari na yale ya kuandaa andalio na azimio la kazi. Uchambuzi zaidi uliofanyika katika majibu ya watahiniwa ulibaini kuwa baadhi ya watahiniwa walibainisha kwa usahihi jambo moja kati ya manne yaliyotakiwa kwenye swali. Jambo lililobainishwa na watahiniwa hao ni *zana za kufundishia*. Hii inaweza kusababishwa na watahiniwa kuweka

kumbukumbu kwa sababu jambo hili kufanywa na walimu wakati wa kufundisha na kujifunza. Kielelezo Na. 6.2 kinaonesha sampuli ya jibu ambalo siyo sahihi kutoka kwa mmoja wa watahiniwa.



6 Mwalimu anapochambua muhtasari anataki wa:
(i) Kuchambua jalada la muhtasari huo
(ii) Kuchambua mwaka ulioandikwa muhtasari huo.
(iii) Kuchambua hati miliki wa muhtasari.
(iv) Kuchambua yaliyomo katika muhtasari

Kielelezo Na. 6.2: Sampuli ya jibu la swali la 6 ambalo siyo sahihi.

Kielelezo Na. 6.2 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyebainisha mambo anayopaswa kuzingatiwa mwalimu wa somo la TEHAMA anapotaka kuchagua muhtasari wa somo.

### 2.1.7 Swali la 7: Maandalizi ya Ufundishaji na Ujifunzaji wa Somo la TEHAMA


Katika swali hili, mtahiniwa alitakiwa kueleza kwa ufupi faida nne za tathmini kama kipengele muhimu katika andalio la somo. Watahiniwa wote 3,698 (100%) walifanya swali hili; kati yao watahiniwa 3,669 (99.2%) walipata alama kuanzia 3 hadi 4. Aidha, takwimu zinaonesha kuwa watahiniwa 13 (0.4%) walipata alama kuanzia 2 hadi 2.5 na watahiniwa 16 (0.4%) walipata alama 0 hadi 1.5. Kwa ujumla, swali hili lilikuwa na kiwango kizuri cha ufaulu kwa sababu asilimia 99.6 ya watahiniwa wote walipata alama zaidi ya 1.5 kama inavyooneshwa kwenye Chati Na. 5.




**Chati Na. 5:** *Ufaulu kwa watahiniwa katika swali la 7.*

Watahiniwa wengi walieleza kwa ufasaha faida za tathmini katika andalio la somo. Kiwango hiki kizuri cha ufaulu huenda kilisababishwa na ukweli kwamba tathmini kwa njia mbalimbali zinatumika kupima mafanikio na maendeleo ya mwanachuo. Njia hizo ni pamoja na majaribio, vitendo, kazi binafsi, mitihani ya muhula na mitihani ya kitaifa; hivyo watahiniwa walihawilisha kwa urahisi maarifa ya tathmini katika maandalizi ya somo.

Majibu yaliyoelezwa na watahiniwa kwa ufasaha ni pamoja na; Humwezesha *mwalimu kutambua namna somo lilivyoeleweka au kutoeleweka, husaidia kubaini mapungufu ya mwalimu katika ufundishaji* na *husaidia kujua mafanikio na matatizo yaliyojitokeza katika ufundishaji*. Hoja nyingine iliyoelezwa ni: *husaidia kujua ugumu wa mada iliyofundishwa*. Watahiniwa walidhihirisha kuwa na maarifa ya kutosha kuhusu faida za tathimini. Kielelezo Na. 7 kinaonesha jibu sahihi kutoka kwa mmoja wa watahiniwa.


7 Zifuatazo ni faida nne za tathmini kama kipengele muhimu katika andalio la somo.

(i) Humsaidia mwalimu kupima kufikiwa kwa malengo au kutokufikiwa kwa malengo

(ii) Humsaidia mwalimu kuboresha njia na mbinu za ufundishaji

(iii) Humsaidia mwalimu kubainisha mapungufu yanayojitokeza katika ufundishaji na ujifunzaji wa somo.

(iv) Humsaidia mwalimu kutambua uwezo wa wanafunzi kitaaluma

Kielelezo Na. 7: Sampuli ya jibu sahihi katika swali la 7.

Kielelezo Na. 7, kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyeeleza kwa usahihi faida nne za tathmini kama kipengele muhimu katika andalio la somo.

Hata hivyo, watahiniwa wachache ambao hawakuwa na kiwango kizuri cha ufaulu walieleza kwa usahihi hoja moja wengine mbili kati ya nne na zingine hazikuwa sahihi. Uchambuzi zaidi umebaini kuwa, baadhi yao walitoa maelezo ambayo hayajitoshelezi.

### 2.1.8 Swali la 8: Ufundishaji wa Mada za Mfano

Swali hili lilitungwa kutoka katika mada ya *Ufundishaji wa Mada za Mfano* kipengele cha Maktaba. Swali hili lililenga kupima maarifa ya watahiniwa katika kupanga maandiko katika maktaba kwa kufuata maudhui ya andiko. Watahiniwa walitakiwa kueleza kwa kifupi namna nne zinazoweza kutumika kupanga maandiko katika maktaba kwa kufuata maudhui ya andiko.


Jumla ya watahiniwa 3,696 (99.9%) walifanya swali hili, kati yao watahiniwa 33 (0.9%) walipata alama kuanzia 3 hadi 4. Watahiniwa 9 (0.2%) walipata alama kuanzia 2 hadi 2.5 na watahiniwa 3,654 (98.9%) walipata alama 0 hadi 1.5. Uchambuzi wa takwimu unaonesha kuwa watahiniwa 3,607 (97.6%) walipata alama sifuri katika swali hili. Takwimu hizi zinaonesha kuwa kiwango cha ufaulu cha watahiniwa ni hafifu kwa

sababu asilimia 98.9 ya watahiniwa walipata alama chini ya 2 kama inavyooneshwa katika Jedwali Na. 2.

**Jedwali Na.3: Ufaulu wa Watahiniwa Katika Swali la 8**

| Alama | Idadi ya Watahaniwa | Asilimia ya Watahiniwa |
|---|---|---|
| 0 - 1.5 | 3,654 | 98.9 |
| 2.0 - 2.5 | 9 | 0.2 |
| 3.0 - 4.0 | 33 | 0.9 |

Swali hili ni miongoni mwa maswali yenye kiwango hafifu cha ufaulu. Watahiniwa wengi 3,607 (97.6%) waliopata alama 0 katika swali hili hawakuwa na uelewa wa kutosha juu ya upangaji wa maandiko katika maktaba. Baadhi yao hawakuelewa matakwa ya swali hivyo, walibuni majibu mbalimbali. Kwa mfano baadhi ya watahiniwa waliandika *kupanga maandiko kwa kuzingatia jina la andiko, mada ya andiko na mwandishi wa andiko.* Aidha, wengine walieleza *kupanga kwa kufuata alafabeti kuanzia A mpaka Z.* Uchambuzi zaidi unaonesha kuwa baadhi ya watahiniwa walieleza kwa ujumla majibu ambayo ni jumuishi kinyume na matakwa ya swali. Kwa mfano, baadhi ya watahiniwa walieleza *kupanga kulingana na masomo, ubora wa maandiko, kupanga kulingana na kiwango cha elimu ya mhusika.* Kielelezo Na. 8 kinaonesha sampuli ya jibu lisilo sahihi kutoka kwa mmoja wa watahiniwa katika swali hili.




Kielelezo Na. 8: Sampuli ya jibu lisilo sahihi katika swali la 8.

Kielelezo Na. 8, kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kutofautisha jinsi ya kupanga maandiko na habari.

Kwa upande mwingine, watahiniwa wachache 9 (0.2%) waliofaulu kwa kiwango kizuri walielewa matakwa ya swali lakini walikosa maarifa ya kutosha juu ya upangaji wa vitabu katika maktaba. Jambo hili lilisababisha kutokutoa majibu yote kwa ufasaha. Watahiniwa hawa walieleza kwa usahihi angalau namna mbili lakini wakakosea zingine zilizobaki.

Takwimu za majibu ya watahiniwa zinaonesha kuwa, watahiniwa 26 (0.7%) walijibu swali hili kwa ufasaha na kupata alama zote 4. Watahiniwa hawa walikua na maarifa ya namna ya upangaji wa maandiko katika maktaba yaliyowawezesha kujibu swali hilo kwa ufasaha. Miongoni mwa majibu yaliyotolewa na watahiniwa ni: "*Teknolojia- wakati wa kupanga maandiko katika maktaba kwa kufuata maudhui ya teknolojia, lugha- kupanga maandiko kutokana na lugha, historia- kupanga kufuata andiko la maudhui ya historia, Sayansi- maandiko kupangwa kufuata maudhui ya sayansi".*

### 2.1.9 Swali la 9: Ufundishaji wa Mada za Mfano


Swali hili lilitungwa kutoka mada ya Ufundishaji wa Mada za Mfano na lilimtaka mtahiniwa kutofautisha habari inayotolewa kwa njia ya redio na ile inayotolewa kwa njia ya luninga. Watahiniwa 3,698 (100%) walifanya swali hili, kati yao watahiniwa 938 (25.4%) walipata alama kuanzia 3 hadi 4. Takwimu zinaonesha kuwa watahiniwa 540 (11.4%) walipata alama kuanzia 2 hadi 2.5 na watahiniwa 2,220 (60%) walipata alama 0 hadi 1.5. Jedwali Na.4 linaonesha ufupisho wa kiwango cha ufaulu kwa watahiniwa katika swali hili.

**Jedwali Na.4: Ufaulu wa Watahiniwa Katika Swali la 9**

| Alama | Idadi ya Watahaniwa | Asilimia ya Watahiniwa |
|---|---|---|
| 0 - 1.5 | 2,220 | 60.0 |
| 2.0 - 2.5 | 540 | 14.6 |
| 3.0 - 4.0 | 938 | 25.4 |

Kwa ujumla, kiwango cha ufaulu cha watahiniwa katika swali hili kilikuwa cha wastani kwa sababu asilimia 40 ya watahiniwa walipata alama zaidi ya 1.5 kama inavyoonekana katika Jedwali Na.4. Uchambuzi uliofanyika kwenye majibu ya watahiniwa (60%) waliopata alama 0 hadi 1.5 ulibaini kuwa, asilimia 56.6 ya watahiniwa walitoa tofauti sahihi moja tu. Jibu lililotolewa na watahiniwa hao ni: *habari inayotolewa na redio hutolewa kwa njia ya sauti pekee wakati television hutoa habari kwa njia ya sauti na picha*. Takwimu hizi zinaonesha kuwa watahiniwa hawakuwa na uelewa wa


kina kuhusu habari zinazotolewa kwa njia ya redio na luninga. Aidha, baadhi ya watahiniwa walikuwa na uelewa juu ya redio na luninga lakini walishindwa kutoa maelezo bayana yanayotofautisha njia hizo. Kwa mfano baadhi yao waliandika: *redio hutoa habari kwa njia ya picha wakati televisheni hutoa habari inayoeleweka kwa urahisi.* Sampuli ya jibu ambalo siyo sahihi kutoka kwa mmoja wa watahiniwa imeoneshwa kwenye Kielelezo Na. 9.1.


9 Habari inayotolewa kwa njia ya redio
Hit hutolewa kwa njia ya sauti tu bila pi
cha. pia habari hii Msikilizaji husikia bila kuona
Mtoa habari au Matukio ya habari hiyo inayotole
wa, pia haina gharama. Mfano. Redio one, TBC FM

Kielelezo Na. 9.1: Sampuli ya jibu lisilo sahihi katika swali la 9.

Katika Kielelezo Na. 9.1, mtahiniwa alikuwa na uelewa juu ya habari inayotolewa kwa njia ya redio lakini alishindwa kutoa maelezo ya habari inayotolewa kwa njia ya television.

Hata hivyo, watahiniwa 938 (25.4%) waliofaulu kwa kiwango kizuri walikuwa na uelewa mzuri juu ya habari zinazotolewa kwa njia ya redio na telesisheni kwani walijibu kwa ufasha kulingana na matakwa ya swali. Aidha, baadhi yao walikosa maarifa ambayo yangewawezesha kutoa maelezo kwa ufasaha. Watahiniwa hao waliweza kujibu baadhi ya tofauti kwa usahihi na nyingine si sahihi. Sampuli ya jibu sahihi katika swali hili imeoneshwa katika Kielelezo Na. 9.2.




| | | |
|---|---|---|
| 9 | Habari kwa njia ya Redio | Habari kwa njia ya tolev shoni. |
| i/ | Hutumia Sauti katika kuwasilisha habari. | - Hutumia picha, Sauti na Maandishi katika kuwasilisha habari. |
| ii/ | Huhusisha Mlango mmoja wa fahamu ambayo ni Masikio katika kusikiliza | - Huhusisha Milango miwili ya fahamu katika kupata habari mfano Macho kuona picha na Masikio. |
| iii/ | Huleta Ubaguzi katika kupata habari au taarifa Mfano Viziwi hawezi kusikiliza | - Haileti Ubaguzi kwa kuwa hata Viziwi wanaweza kutua tisha mdomo wa mtoa habari na kupata Maana ya habari |
| iv/ | Huwezi kuona Matukio kwa Vitendo ya habari au taarifa unayopata | - Habari na taarifa inayotolewa huona kwa Vitendo Vinavyofanyika. |

Kielelezo Na. 9.2: Sampuli ya jibu sahihi katika swali la 9.

Kielelezo Na. 9.2, kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyetofautisha kwa usahihi habari inayotolewa kwa njia ya redio na ile inayotolewa kwa njia ya televisheni.

### 2.1.10 Swali la 10: Ufundishaji wa Mada za Mfano


Swali hili lililenga kupima maarifa waliyonayo watahiniwa katika kubaini na kuelezea michoro ya alama za barabarani. Swali hili lilimtaka mtahiniwa kubainisha michoro minne inayochorwa barabarani na kisha kuonesha taarifa inayotoa kwa mtumiaji wa barabara.Watahiniwa 3,696 (99.9%) walifanya swali hili, ambapo watahininiwa 153 (4.1%) walipata alama kuanzia 3 hadi 4. Aidha, watahiniwa 486 (13.2%) walipata alama kuanzia 2 hadi 2.5 na watahiniwa 3,055 (82.7%) walipata alama 0 hadi 1.5. Kwa ujumla, kiwango cha watahiniwa cha ufaulu ni hafifu kwa sababu watahiniwa 639 (17.3%) walipata alama zaidi ya 1.5. Chati Na.6 inaonesha kiwango cha ufaulu kwa watahiniwa katika swali hili.




**Chati Na. 6:** *Ufaulu kwa watahiniwa kwa asilimia katika swali la 10.*

Chati Na. 6 inaonesha kuwa, asilimia 82.7 ya watahiniwa walipata alama 0 hadi 1.5, kati yao watahiniwa 1,480 (40.1%) walipata alama 0. Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa, watahiniwa wengi hawakuweza kutofautisha alama zinazochorwa kwenye barabara na zile zinachorwa kwenye mabango yaliyoko pembezoni mwa barabara.

Watahiniwa wengi walichora na kueleza alama ambazo huwekwa kwenye vibao. Kwa mfano, baadhi ya watahiniwa walichora na kueleza alama za *Hospitali (H), mwendo wa Km 50 kwa saa, daraja, mteremko mkali* na *mzunguko*. Watahiniwa hawa walitakiwa kubainisha na kuchora alama zinazochorwa kwenye barabara kama vile, kivuko cha watembea kwa miguu (Pundamilia), Michoro ya pinda kushoto au kulia, simama na mstari wa kutenganisha uelekeo wa magari ya abilia. Hata hivyo, baadhi ya watahiniwa walibainisha alama ambazo huchorwa kwenye mabango na kwenye barabara lakini hawakutoa maelezo yanayojitosheleza. Kwa mfano, baadhi yao walibainisha alama ya *Stop* na wengine walichora alama ya watembea kwa miguu (pundamilia). Kielelezo Na. 10 kinaonesha sampuli ya jibu lisilo sahihi kutoka kwa mmoja wa watahiniwa.




Kielelezo Na. 10: Sampuli ya jibu ambalo siyo sahihi.

Katika kielelezo Na. 10, mtahiniwa alichora michoro inayoonesha mabango ya alama zinazowekwa barabarani na taa za barabarani kinyume na matakwa ya swali.


Watahiniwa wachache 486 (13.2%) walibainisha michoro angalau miwili na kutoa maelezo ya taarifa inayotoa kwa mtumiaji wa barabara kwa usahihi. Wengine walibainisha michoro kwa usahihi lakini hawakutoa maelezo ya kina ya taarifa inazotoa kwa mtumiaji wa barabara. Hii inadhihirisha kwamba watahimiwa hawa walielewa matakwa ya swali lakini hawakuwa na maarifa yakutosha juu ya alama zinazochorwa kwenye barabara.

## 2.2 SEHEMU B

Sehemu B ilikuwa na jumla ya maswali sita (6) ya insha yenye jumla ya alama 60 ambapo mtahiniwa alitakiwa kuchagua maswali manne tu. Katika sehemu hii kila swali lilikuwa na alama kumi na tano (15). Kiwango cha ufaulu cha watahiniwa kiligawanywa katika makundi matatu kulingana na alama walizopata. Watahiniwa waliopata alama 0 hadi 5.5 walihesabiwa katika kundi la watahiniwa wenye kiwango hafifu cha ufaulu na alama kuanzia 6 hadi 10 kiwango cha wastani cha ufaulu. Aidha, watahiniwa waliopata alama kuanzia 10.5 hadi 15 walihesabika kuwa na kiwango kizuri cha ufaulu.

### 2.2.1 Swali la 11: Misingi ya Ufundishaji na Ujifunzaji wa Somo la TEHAMA

Swali hili lililenga kupima uwezo wa watahiniwa katika kutathmini mchango wa msingi wa ufundishaji unaompa mwanafunzi uwezo wa kutafuta, kuchambua na kuwasilisha habari na taarifa. Mtahiniwa alitakiwa kutathmini kwa kutoa hoja 5. Watahiniwa 2,671 (72.2%) walifanya swali hili; kati yao watahiniwa 539 (20.2%) walipata alama kuanzia 10.5 hadi 15 na watahiniwa 1,395 (52.2%) walipata alama kuanzia 6 hadi 10. Watahiniwa waliopata alama 0 hadi 5.5 walikuwa 737 sawa na asilimia 27.6. Chati Na. 7 inaonesha ufaulu kwa watahiniwa katika swali hili.





**Chati Na. 7:** *Ufaulu kwa watahiniwa kwa asilimia katika swali la 11.*

Kiwango cha ufaulu cha watahiniwa katika swali hili ni kizuri kwa sababu asilimia 72.4 ya watahiniwa walipata alama kuanzia 6 hadi 15 kama ilivyooneshwa kwenye Chati Na.7. Ingawa swali hili ni miongoni mwa maswali yenye kiwango kizuri cha ufaulu watahiniwa wengi (52.2%) walipata alama za wastani kuanzia 6 hadi 10. Baadhi ya watahiniwa hawa walitoa utangulizi sahihi na hoja sahihi mbili au tatu kati ya tano. Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa ulibaini kuwa, watahiniwa wengine walitoa hoja bila maelezo yanayojitosheleza jambo lililosababisha kupoteza alama. Hoja za kutathimini zilizotolewa na watahiniwa wengi ni: *huongeza*

*ushirikiano wa mwanafunzi na wenzake na huongeza stadi za kujiamini kwa mwanafunzi*.

Watahiniwa waliopata alama 0 hadi 5.5 walishindwa kuelewa matakwa ya swali kwa sababu majibu waliyotoa hayakuonyesha tathmini ya msingi wa ufundishaji unaompa mwanafunzi uwezo wa kutafuta, kuchambua na kuwasilisha habari na taarifa. Uchambuzi uliofanyika katika majibu ya watahiniwa ulionyesha kuwa, baadhi yao waliandika majibu kwa kutumia maneno kutafuta, kuchambua na kuwasilisha habari na taarifa. Kwa mfano, baadhi ya watahiniwa waliandika: *mwanafunzi anapata stadi za kuchambua habari, stadi za kutafuta habari, stadi za kuwasilisha habari na stadi za kuwasilisha taarifa.* Wengine waliandika: *msingi wa ufundishaji unampa mwanafunzi uwezo wa kutafuta vyanzo vya habari, kutafsiri habari na kutumia vifaa vya TEHAMA.* Majibu haya ya watahiniwa yanaonyesha kuwa, watahiniwa walishindwa kuelewa maana ya kauli kitenzi “tathmini” iliyotumika kwenye swali hivyo, kutoa majibu kinyume na matakwa ya swali. Hata hivyo, baadhi yao walitoa hoja moja sahihi lakini walishindwa kutoa hoja zingine. Hoja iliyotolewa na wanafunzi wengi ni *kumjengea mwanafunzi uwezo wa kujenga kumbukumbu za kudumu kwa mwanafunzi*. Kielelezo Na. 11 kinaonesha sampuli ya jibu ambalo siyo sahihi kutoka kwa mmoja wa watahiniwa.


11. Tathimini mchango wa msingi wa Ufundishaji Unaompa mwanafunzi Uwezo wa Kutafuta
Zifuatazo ni msingi ya Ufundishaji na Ujifunzaji Unaompa mwanafunzi Uwezo wa kutafuta.
Ufundishaji Unaozingatia Vitendo; Katika Ufundishaji na Ujifunzaji kwa Vitendo humjengea mwanafunzi Uwezo kufanya kitu kwa Ustadi mkubwa.
Ufundishaji na Ujifunzaji unaochochea Udadisi Unaoleta maana ya kitu anachojifunza; Katika Ufundishaji na Ujifunzaji humsaidia mwanafunzi Udadisi wa kitu alichojifunza
Ufundishaji na Ujifunzaji Unaozingatia Usalama wa wanafunzi na Vifaa vya kufundishia na kujifunzia Katika Ufundishaji na Ujifunzaji ni lazima kuzingatia Usalama wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia ili kuweza kutoa watoa wanafunzi wakati wa ufundishaji na Ujifunzaji
Ufundishaji na Ujifunzaji Unaozingatia matumizi ya vifaa vya tehama; Katika Ufundishaji na Ujifunzaji wa somo la tehama Unazingatia sana matumizi ya Vifaa vyake katika Ufundishaji na Ujifunzaji
Ufundishaji na Ujifunzaji Unaozingatia Usafi wa jinsia na manwala ya mtambiko; Katika Ufundishaji na Ujifunzaji wa somo la Tehama mwanafunzi kujua Usafi wa jinsia na manwala ya mtambiko
Hivyo basi msingi ya Ufundishaji na Ujifunzaji Unampa mwanafunzi Uwezo wa kutafuta na kujua mambo mengi katika kujisomea na kujifunza pia

Kielelezo Na. 11: Sampuli ya jibu lisilo sahihi katika swali la 11.

Katika kielelezo Na. 11, mtahiniwa alitoa hoja kwa kueleza aina za ufundishaji badala ya kufanya tathimini ya mchango wa ufundishaji katika kutafuta, kuchambua na kuwasilisha habari.

Aidha, watahiniwa waliopata alama kuanzia 10.5 hadi 15 walifanya tathmini sahihi ya mchango wa msingi wa ufundishaji unaompa mwanafunzi uwezo wa kutafuta kuchambua na kuwasilisha habari na taarifa. Watahiniwa hao walionesha kuelewa matakwa ya swali na hivyo kujibu swali kwa ufasaha. Watahiniwa hawa walitoa hoja kama: *humjengea mwanafunzi uwezo wa kujieleza, humjengea mwanafunzi hali ya udadisi, humjengea mwanafunzi uwezo wa kujieleza, humjengea mwanafunzi uwezo wa kuthubutu,*

*humjengea mwanafunzi uwezo wa kujiamini*. Hata hivyo, baadhi yao hawakutoa maelezo yanayojitosheleza katika hoja walizotoa.

### 2.2.2 Swali la 12: Ufundishaji wa Mada za Mfano

Swali hili lilitoka katika mada ya Ufundishaji wa Mada za Mfano. Mtahiniwa alipimwa umahiri wa kufafanua kwa kina mambo matano yanayoweza kuathili uwasilishaji wa habari iliyosemwa kwa kutoa mifano halisi. Watahiniwa 2,802 (75.8%) walifanya swali hili ambapo watahiniwa 430 (15.4%) walipata alama kuanzia 10.5 hadi 15 na watahiniwa 1,968 (70.2%) walipata alama kuanzia 6 hadi 10. Uchambuzi wa takwimu unaonesha, watahiniwa 404 (14.4%) walipata alama kuanzia 0 hadi 5.5. Ufupisho wa kiwango cha ufaulu umeoneshwa katika Jedwali Na. 5.

**Jedwali Na.5: Ufaulu wa Watahiniwa Katika Swali la 9**

| Alama | Idadi ya Watahaniwa | Asilimia ya Watahiniwa |
|---|---|---|
| 0 - 5.5 | 404 | 14.4 |
| 6.0 – 10.0 | 1,968 | 70.2 |
| 10.5 – 15.0 | 430 | 15.4 |

Kwa ujumla swali hili lilikuwa na kiwango kizuri cha ufaulu kwa sababu asilimia 85.6 ya watahiniwa walipata alama zaidi ya 5.5. Uchambuzi uliofanyika kwenye sampuli ya majibu ya watahiniwa (70.2%) waliopata kiwango cha wastani cha ufaulu ulionyesha kuwa wote walikuwa na uelewa wa mambo yanayoweza kuathiri uwasilishaji wa habari iliyosemwa. Hata hivyo, walishindwa kufafanua kwa kina majibu yao na wengine walishindwa kutoa mifano halisi. Aidha, watahiniwa wengine walitoa hoja zenye kujirudia rudia kama vile: *uwepo wa makelele wakati habari inawasilishwa na kutokuwepo kwa usikivu, Ulemavu na athari za kimaumbile*.

Pamoja na watahiniwa wengi ufaulu kwa kiwango cha wastani, asilimia 15.4 ya watahiniwa walifaulu kwa kiwango kizuri kwani walipata alama 10.5 hadi 15. Baadhi ya watahiniwa hawa walifafanua kwa usahihi mambo yanayoathiri uwasilishaji wa habari iliyosemwa lakini walishindwa kutoa mifano halisi katika baadhi ya hoja zao. Kwa mfano, baadhi ya watahiniwa waliandika: *Athari za kimaumbile katika ogani za matamshi, athari za lugha mama katika uwasilishaji habari, tatizo la kutosikia vizuri, maneno kuwa na maana zaidi ya moja, muwasilishaji kuwa na tatizo la kigugumizi*.

Kielelezo Na. 12.1 kinaonesha sampuli ya jibu sahihi kutoka kwa mmoja wa watahiniwa.

12. Uwasilishaji wa habari iliyosemwa ni
ile hali ya kuwasomea wanafunzi au kuwa
sikilizisha toka katika rekodi mbalimbali ili
kuweza kusikia habari iliyosemwa kwa u
fanisi zaidi. Katika habari iliyosemwa
kuna mambo ambayo yanaweza kuathiri
kutokana na habari hiyo kuwasilishwa.
Yafuatayo ni mambo yanayoweza kua
thiri habari inayosemwa au iliyosemwa ka
ma ifuatavyo.
Athari za Lugha mama; Hii ni moja y
tatizo kubwa katika uwasilishaji wa mad
iliyosemwa kwa sababu kuna maneno ya
tatamkwa lakini msikilizaji atashindwa
kuyatafsiri kulingana na msomaji kuathi
riwa na Lugha mama mfano wa maneno
Sindano — shindano.
Lala — Rata
kula — kura
ulemavu katika viungo vya ala za saut
Hii ni moja ya athari ambazo huweza ku
athiri uwasilishaji wa habari iliyosemwa
kama msemaji wa habari hiyo atatamk
baadhi ya maneno tofauti na yana maa
na moja bila kuitofautisha. kwa mfano.
Neno Balabara — barabara
Chakula — Chakura

12 kutokusikia vizuri (uziwi)! Hii ni hali ya msemaji wa habari au mwasilishaji wa habari au msikilizaji kutokusikia vizuri kile kinachosemwa ambapo itampelekea kushindwa kuelewa mada inayosemwa. Hii ni moja ya kuathiriwa na uziwi kwa mfano Nero mama anapika ugali yeye atauliza anafanyaje? na kumpelekea msomaji kurudia rudia kusoma habari iliyosemwa.

Mwasilishaji kuwa na kithembe, Hii ni moja ya athari katika kuwasilisha habari iliyosemwa kwani msemaji kwa maneno atayatamka kwa kugugumia ambapo itapelekea wasikilizaji kushindwa kuelewa habari iliyosemwa kwa mfano, Nero. Baba - yeye atasema a-ba-ba itapelekea habari kutosikiwa vizuri.

Kasoro katika matamshi ya baadhi ya silabi! Hii hutokana na lugha mama pia ambapo mtamkaji au mwasilishaji atatamka matamshi siyo kwa ufasaha itampelekea kushindwa kueleweka kwa wasikilizaji wake. Kwa mfano. Baba analima na mama amelala yeye atasema Analima baba na Mama amerara.

Kielelezo Na. 12.1: Sampuli ya jibu sahihi katika swali la 12.

Katika kielelezo Na. 12.1, mtahiniwa alifafanua kwa usahihi pia alitumia mifano ya mambo yanayoathiri uwasilishaji wa habari.

Kwa upande mwingine, watahiniwa (14.4%) walifaulu kwa kiwango hafifu kutokana kutokuwa na maarifa ya kutosha pamoja na kutoelewa matakwa ya swali. Ilibainika kuwa, baadhi ya watahiniwa walifafanua mambo yanayoonesha changamoto za uwasilishaji wa habari katika vyombo mbalimbali vya habari badala ya mambo yanayoathiri uwasilishaji habari iliyosemwa. Kwa mfano baadhi yao waliandika kuwa: *kupata mawasiliano na waandishi wa habari, gharama za kulipia habari unayotaka irushwe na*

*vyombo vya habari*. Aidha, baadhi yao walifafanua kwa usahihi hoja moja au mbili lakini walichanganya na hoja ambazo hazikuwa matakwa ya swali. Kwa mfano, mmoja wa watahiniwa aliandika: *Muwasilishaji kuwa na sauti ndogo, tarehe ya kuwasilisha habari na jamii inayopokea habari*. Kielelezo Na.12.2 kinaonesha sampuli ya jibu la mtahiniwa lenye makosa.

12. Habari ni taarifa au ujumbe unaotolewa kuhusu jambo au mada fulani. Ambapo habari ili iweze kutolewa kwa wahusika lazima iwe imefanyiwa uchunguzi kuzi kina na kwa weledi.

Uwasilishwaji wa habari iliyosemwa unaweza kuathiriwa na mambo kadhaa, baadhi ya mambo hayo ni:

Habari inayotolewa kama haijafanyiwa utafiti au uchunguzi kwa kina uweza kupotosha jamii, mfano magazeti, iwapo magazeti yaliyoandika hayajafanyiwa uchunguzi kwa kina habari inayotolewa inaweza kupotosha jamii.

Redio, matangazo yanayotolewa au yanayotangazwa kwenye redio kama waandishi hawajafanya upelelezi zaidi wa habari hiyo, habari inayotolewa inaweza kuwa habari za uongo.

Mtandao, huu ni mfumo wa kisasa mkubwa sana katika mawasiliano unaoshirikiana na kompyuta katika kurahisisha mawasiliano, ambapo habari nyingi kabla hazijatolewa kwenye vyombo vya habari tayari habari hiyo inakuwa isharushwa kwenye mtandao. hivyo habari hiyo isipofanyiwa utafiti kwa undani inaweza kuathiri uwasilishaji wa habari inayosemwa.


Majarida, ni nakala mbalimbali kama kitabu ambazo uandikwa na kutiwa na jarida, juu, ambapo habari za majarida ufanyiwa utafiti na watu wenye ujuzi na elimu ya kuandika majarida mfano maprofesa. hivyo waandishi wanapaswa utafiti kwa kina kuhusu habari inayotakiwa kutolewa.

Kielelezo Na. 12.2: Sampuli ya jibu ambalo siyo sahihi katika swali la 12.

Kielelezo Na. 12.2 kinaonesha mtahiniwa aliyefafanua njia za mawasiliano zinazoweza kufikisha habari badala ya mambo yanayoweza kuathili uwasilishaji wa habari iliyosemwa.

### 2.2.3 Swali la 13: Upimaji

Swali hili lililenga kupima uwezo wa watahiniwa katika kutathmini zana mbalimbali za upimaji zinazotumika kumchunguza mwanafunzi wakati wa ufundishaji na ujifunzaji wa somo la TEHAMA. Katika swali hili, mtahiniwa alitakiwa kujadili kwa hoja tano kwa kutoa mifano dhahiri juu ya kauli "ili tendo la ufundishaji na ujifunzaji wa somo la TEHAMA likamilike, mwalimu hana budi kumchunguza mwanafunzi kwa kutumia zana mbalimbali". Takwimu zinaonesha kuwa, watahiniwa 2,876 (77.8%) walifanya swali hili, kati yao watahiniwa 1,652 (57.4%) walipata alama kuanzia 10.5 hadi 15. Watahiniwa 879 (30.6%) walipata alama kuanzia 6 hadi 10 na watahiniwa 345 (12.0%) walipata alama 0 hadi 5.5. Chati Na. 8 inaonesha ufupisho wa mchanganuo wa kiwango cha ufaulu katika swali hili.




**Chati Na. 8:** *Ufaulu kwa watahiniwa kwa asilimia katika swali la 13.*

Kwa jumla, kiwango cha watahiniwa cha ufaulu katika swali hili kilikuwa kizuri kwa sababu asilimia 88.0 ya watahiniwa walipata alama zaidi ya 5.5. Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa ulionesha kuwa, watahiniwa waliopata alama kuanzia 10.5 hadi 15 walijadili hoja kwa usahihi lakini wengi wao hawakutumia mifano dhahiri wakati wa kujadili. Vilevile baadhi

ya watahiniwa walitoa hoja kwa usahihi bila kuandika utangulizi wala hitimisho. Miongoni mwa hoja zilizojadiliwa ni pamoja na: *Mazoezi mbalimbali, majaribio, mitihani na hojaji.* Kielelezo Na. 13.1 kinaonesha sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyejibu swali kwa usahihi.

13 Zana za Uchunguzi Kwa Mwanafunzi - Ni
jumla ya njia zinazotumika kumchunguza
Mwanafunzi kiwango cha Maarifa aliyopata baada
ya kujifunza mada fulani au kumalizika kwa
Mada hiyo. Ni kweli ili tendo la Ufundishaji na
Ujifunzaji wa somo la TEHAMA likamilike mwalimu
anapaswa kumchunguza Mwanafunzi kwa kutumia
zana mbalimbali kama zifuatazo.
Mazoezi mbalimbali: Ili ufundishaji uka-
milike mwalimu anapaswa kumchunguza mwanafunzi
kwa kutumia mazoezi darasani baada ya ufundishaji
katika kila kipindi. Hii husaidia kuelewa ni kwa
kiwango gani malengo ya kipindi husika yamefikiwa
au hayajafikiwa hivyo mwalimu anaweza kutumia
zana hii ya upimaji kumpima Mwanafunzi
Majaribio: Mwalimu hana budi kutumia
Zana hii kuchunguza Mwanafunzi katika tendo la
Ufundishaji na Ujifunzaji. Majaribio yanaweza kutolewa
baada ya mada kukamilika au katikati ya mada
au kukamilika kwa mada zaidi ya moja. pia
yanaweza kumchunguza mwanafunzi kila mwisho
wa wiki hii husaidia Mwalimu kupima uwezo
wa Mwanafunzi katika Mada fulani.
Mitihani: Mwalimu anaweza kutumia
Zana hii kumchunguza Mwanafunzi katika
kukamilisha tendo zima ufundishaji na ujifunzaji.
Hii utolewa baada ya Mada kadhaa kukamilika
pia utolewa ndani ya robo muhula, nusu muhula,
Muhula mzima au mwaka mzima ambayo husaidia
kufahamu maendeleo ya Mwanafunzi kitaaluma.
Hojaji - Mwanafunzi pia anaweza

| | |
|---|---|
| 13 | Kuchunguzwa kwa kutumia hoja kwa kuulizana |
| | maswali ya ana kwa ana baina ya Mwanafunzi na |
| | Mwalimu baada ya kipindi fulani hii pia inasaidia |
| | kujua kama mwanafunzi ameelewa au hajaelewa. |
| | Muongozo wa Usaili. Ni zana nyingine |
| | ya uchunguzi kwa Mwanafunzi kutoka Mchakato |
| | mzima wa ufundishaji na ujifunzaji haya ni |
| | Maswali ambayo uandaliwa na Mwalimu kisha |
| | kuulizwa kwa mwanafunzi mmojammoja. |
| | Kwakutumia zana hizo husaidia mwalimu |
| | kujua kama ufundishaji umekamilika au ujakamilik |
| | kutokana na matokeo atakayoyapata kwa wana |
| | funzi yanaweza kumruhusu kuendelea na sehemu |
| | nyingine au kurudia sehemu hiyo pia humsaidia |
| | kujua ubora wa mbinu na zana za kufundishia |
| | na kujifunzia hivyo ni Ujema Mwalimu kufany |
| | upimaji. |


Kielelezo Na. 13.1: Sampuli ya jibu sahihi kwa swali la 13.

Katika kielelezo Na. 13.1, mtahiniwa alijadili kwa usahihi zana mbalimbali anazotakiwa kutumia mwalimu kumchunguza mwanafunzi.

Pamoja na watahiniwa wengi ufaulu kwa kiwango kizuri, watahiniwa 879 sawa na asilimia 30.6 walifaulu kwa kiwango cha wastani. Kiwango hiki cha wastani kimesababishwa na watahiniwa kutokuwa na uelewa wa kina juu ya zana mbalimbali anazotakiwa kutumia mwalimu kumchunguza mwanafunzi, hivyo kutoa maelezo yasiyokuwa na mifano dhahiri na pia yasiyojitosheleza. Kwa mfano baadhi yao waliandika: *Mazoezi darasani na majaribio* lakini wakashindwa kutoa mifano ni kwa namna gani mwalimu anaweza kutoa mazoezi na majaribio darasani. Watahiniwa hawa walitakiwa kujua kuwa, mazoezi ya darasani huandaliwa na mwalimu kabla hajafundisha na hutolewa darasani mara baada ya mwalimu kukamilisha ufundishaji wake. Vilevile mwalimu anaweza kuandika zoezi ubaoni, kuwasomea maswali au kuwapa wanakili kutoka katika vitabu vya kiada.

Aidha, asilimia 12 ya watahiniwa waliopata kiwango hafifu cha ufaulu kwa kupata alama 0 hadi 5.5 baadhi yao walishindwa kuelewa matakwa ya swali

kwani walijadili zana za ufundishaji na ujifunzaji badala ya zana mbalimbali anazotakiwa kutumia mwalimu kumchunguza mwanafunzi wakati wa ufundishaji na ujifunzaji. Wengine walijadili aina za zana za ufundishaji na ujifunzaji na wengine kueleza faida za kutumia zana za kufundishia. Kwa mfano, baadhi yao waliandika: *humsaidia mwanafunzi kuelewa haraka, huweka kumbukumbu za kudumu*. Zaidi ya hayo, watahiniwa wachache walitoa utangulizi sahihi na kisha kujadili hoja moja au mbili zinazoweza kutumiwa na mwalimu kumchunguza mwanafunzi wakati wa ufundishaji na ujifunzaji. Kielelezo Na 13.2 kinaonesha sampuli ya jibu ambalo siyo sahihi kutoka kwa mmoja wa watahiniwa katika swali hili.



13. Zana za kufundishia na kujifunzia; Ni vifaa au vitu ambavyo mwalimu hana budi kuvitumia ili kurahisisha suala zima la ufundishaji na ujifunzaji. Mwalimu ambaye hutumia zana mbalimbali katika kujifunza hufanikiwa kufikia lengo la somo kwa muda mwafaka.

Yafuatayo ni mambo yanayoelezea umuhimu wa kutumia zana za kufundishia na kujifunzia.

Humfikirisha mwanafunzi; Mwalimu anapofundisha kwa kutumia zana humfanya mwanafunzi awe katikati cha ujifunzaji hivyo humsaidia mwalimu katika lengo la somo kwa wakati kwa sababu huthiri katika hatua zote. Mfano kutenda kwa vitendo

Huchochea udadisi; Mwanafunzi anaposhiriki katika ujifunzaji huweza kuwa na uwezo wa kudadisi mambo mbalimbali yanayoyaona kwenye zana na kuibua maswali chokozi kwa mwalimu.

Hujenga mahusiano na ushirikiano kwa mwalimu na mwanafunzi; Mwanafunzi anaposhiriki kikamilifu katika kujifunza husababisha kuwa na uhusiano mzuri kati ya mwalimu na mwanafunzi kwa sababu huchochea ari ya ufundishaji na ujifunzaji mfano kushirikiana katika kutafuta majibu.

Hujenga kumbukumbu ya muda mrefu; Matumizi ya zana ni muhimu kwa mwanafunzi kwani mwanafunzi anapotenda wakati wa kujifunza husaidia kutunza kumbukumbu ya muda mrefu kwa sababu huhusisha kuona, kusikia, kugusa na kunusa hivyo haweza kusahau.


Humwezesha mwalimu kuelezea dhana tata kwa wakati; kutokana na kuwepo kwa zana za kufundishia na kujifunzia humsaidia mwalimu kuelezea kitu kigeni kwa wanafunzi kwa

Kielelezo Na. 13.2: Sampuli ya jibu ambalo siyo sahihi katika swali la 13.

Katika kielelezo Na. 13.2, mtahiniwa alijadili mchango wa msingi wa ufundishaji unaompa mwanafunzi uwezo wa kutafuta, kuchambua na kuwasilisha taarifa.

### 2.2.4 Swali la 14: Misingi ya Ufundishaji na Ujifunzaji wa Somo la TEHAMA

Swali hili lilimtaka mtahiniwa kuonesha uhusiano uliopo kati ya zana na ujifunzaji wa mwanafunzi katika somo la TEHAMA. Jumla ya watahiniwa 2,857 (77.3%) walifanya swali hili, kati yao watahiniwa 2,166 (75.8%) walipata alama kuanzia 10.5 hadi 15. Uchambuzi wa takwimu unaonesha kuwa watahiniwa 560 (19.6%) walipata alama kuanzia 6 hadi 10 na watahiniwa 131 (4.6%) walipata alama 0 hadi 5.5. Chati Na. 9 inaonesha ufupisho wa mchanganuo wa kiwango cha ufaulu katika swali hili.




**Chati Na. 9:** *Ufaulu kwa watahiniwa kwa asilimia katika swali la 14.*

Kiwango cha watahiniwa cha ufaulu katika swali hili ni kizuri kwani asilimia 95.4 ya watahiniwa walipata alama zaidi ya 5.5 kama ilivyoonyeshwa kwenye Chati Na.9. Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa katika swali hili unaonesha kuwa asilimia 75.8 ya watahiniwa walikuwa na uelewa wa kutosha juu ya uhusiano uliopo kati ya matumizi sahihi ya zana za kufundishia na kujifunzia. Hii huenda ni kwa sababu masomo mengine pia hutoa mada zinazohusu matumizi ya zana za kufundishia hivyo watahiniwa waliweza kuhawilisha maarifa na iliwawezesha kujibu swali kwa ufasaha. Baadhi ya hoja zilizotolewa ni: *humshirikisha mwanafunzi katika ufundishaji, humfanya mwanafunzi ajifunze kwa vitendo, humjengea*


*mwanafunzi kumbukumbu ya kudumu, huamsha ari na hamasa ya kujifunza na humjengea mwanafunzi ubunifu*. Kielelezo Na.14 kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu swali hilo kwa usahihi.

14. Matumizi sahihi ya zana ni kitendo cha mwalimu kuweza kuhusianisha mada au maudhui ya somo na zana husika kwa kuitumia vizuri na kwa muda husika. Ufuatao ni uhusiano uliopo kati ya matumizi sahihi ya zana na ujifunzaji wa mwanafunzi katika somo la Tehama.

Humshirikisha mwanafunzi. Mwalimu anapotumia zana kwa usahihi lazima amshirikishe mwanafunzi katika ~~utumia~~ ujifunzaji kwa kutumia zana hizo. Kuwahizo hii husaidia mwanafunzi kushiriki vizuri katika ujifunzaji wake.

Mwanafunzi kujifunza kwa vitendo. Matumizi sahihi ya zana humfanya mwanafunzi ajifunze kwa vitendo. Zaidi mfano akiambiwa njia ya kusafishia mwili ni brashi, sabuni na maji alafu mwalimu akamwonyesha na kumpa mwanafunzi nafasi ya kuitazama na kushika.

Humjengea kumbukumbu ya kudumu. Mwalimu anapotumia zana kwa usahihi humjengea mwanafunzi kumbukumbu ya kudumu. Mfano akisema maada imegawanyika katika hali tatu gesi, kimiminika na yabisi alafu akawaonyesha mfano wa maada za hali hizo itakuwa ngumu kwa wanafunzi hao kusahau walichojifunza.



14 Huamsha ari na hamasa ya kujifunza. Mwalimu anapofundisha kwa kutumia zana kwa usahihi, wanafunzi watakuwa na hamasa ya kujifunza. Mfano unapotumia zana za picha na michoro kwa usahihi wanafunzi watavutiwa na somo na kuwa na hamasa.

Humjengea mwanafunzi ubunifu na udadisi. Mwalimu atumiapo zana kwa usahihi wanafunzi hupata au huongeza ujuzi na ubunifu katika kutengeneza vitu kama walivyojifunza. Mfano unapotumia zana kuonyesha mabadiliko ya maada mwanafunzi anaweza kudadisi na kubuni badiliko lolote la kiumbo au kikemikali tofauti na walilofundishwa.

Kwahiyo ni muhimu mwalimu kutumia zana kwa usahihi wakati wa ufundishaji na ujifunzaji

Kielelezo Na. 14: Sampuli ya jibu sahihi katika swali la 14.

Kielelezo Na. 14 kinaonesha mtahiniwa aliyeonesha uhusiano kati ya matumizi sahihi ya zana na ujifunzaji wa mwanafunzi.

Kwa upande mwingine, watahiniwa (19.6%) waliofaulu swali hili kwa kiwango cha wastani walielewa matakwa ya swali lakini walishindwa kuonyesha bayana uhusiano uliopo kati ya matumizi sahihi ya zana na ujifunzaji wa mwanafunzi katika somo la TEHAMA. Wengine waliweza kueleza hoja tatu kwa ufasaha lakini wakashindwa kuelezea hoja zingine zilizobaki. Aidha, baadhi ya watahinwa walionesha uhusiano kati ya zana husika na ujifunzaji wa mwanafunzi bila ufafanuzi unaojitosheleza. Kwa mfano baadhi ya watahiniwa waliandika: *Somo kueleweka kwa urahisi, ni vyepesi mwanafunzi kuelewa somo anapojifunza kwa kutumia zana sahihi. Hata hivyo, endapo kutakuwepo na matumizi mabaya ya zana mwanafunzi anaweza kuchukia somo.* Majibu haya hayaoneshi zana gani inaweza

kutumiwa katika somo la TEHAMA ili kurahisisha ujifunzaji wa mwanafunzi. Watahiniwa wangeweza kutumia zana ya kompyuta kama mfano unaoweza kutumika kumfundishia mwanafunzi kujua sehemu za kompyuta.

Uchambuzi wa majibu ya baadhi watahiniwa (4.6%) waliofaulu kwa kiwango hafifu unaonesha kuwa, walijibu swali hilo kwa kuelezea sifa za zana za kufundishia kinyume na matakwa ya swali. Wengine waliandika umuhimu wa zana za kufundishia kwa ujumla. Kwa mfano, mmoja wa watahiniwa aliandika: *lazima ziendane na mada, umri au uelewa wa mwanafunzi, lazima zichochee udadisi*. Majibu haya ya mtahiniwa yanadhihirisha kuwa, mtahiniwa hakuwa na maarifa ya kutosha na hakuelewa matakwa ya swali. Aidha, baadhi yao walitoa utangulizi na kuhusianisha zana moja sahihi na ujifunzaji wa mwanafunzi.

### 2.2.5 Swali la 15: Ufundishaji wa Mada za Mfano

Swali hili lilipima uwezo wa mtahiniwa kueleza kwa kina jinsi ya kuepuka ajali zinazosababishwa na ukosefu wa alama muhimu za barabarani. Watahiniwa walitakiwa kueleza kwa kutumia hoja tano kujibu swali hili. Watahiniwa 2,705 (73.1%) walijibu swali hili ambapo watahiniwa 1,376 (50.9%) walipata alama kuanzia 10.5 hadi 15 na watahiniwa 1,252 (46.3%) walipata alama kuanzia 6 hdi 10. Uchambuzi wa takwimu unaonesha kuwa, watahiniwa 77 (2.8%) walipata alama 0 hadi 5.5. Jedwali Na.6 linaonesha ufupisho wa kiwango cha ufaulu kwa watahiniwa katika swali hili.

**Jedwali Na.6: Ufaulu wa Watahiniwa Katika Swali la 15**

| Alama | Idadi ya Watahaniwa | Asilimia ya Watahiniwa |
|---|---|---|
| 0 - 5.5 | 77 | 2.8 |
| 6.0 – 10.0 | 1252 | 46.3 |
| 10.5 – 15.0 | 1376 | 50.9 |

Kwa ujumla ufaulu wa watahiniwa katika swali hili ulikuwa mzuri kwa sababu asilimia 97.2 ya watahiniwa walipata alama 6 hadi 15 kama ilivyooneshwa kwenye Jedwali Na.6.

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa asilimia 50.9 ya watahiniwa waliofaulu kwa kiwango kizuri walikua na uelewa ambao uliwawezesha kutoa maelezo ya kina ya namna ya kuepeuka ajali

mbalimbali zinazosababishwa na ukosefu wa alama muhimu za barabarani. Baadhi ya hoja zilizoelezwa na watahiniwa ni: *Kuwa waangalifu wakati wa kuvuka barabara, madereva kuchukua tahadhari zote wakiwa barabarani ikiwemo kutoendesha vyombo vya moto kwa mwendo kasi, serikali kutoa elimu kwa watumiaji wa barabara* na *kuweka askari wa usalama barabarani ili kuongoza magari na watumiaji wengine wa barabara*. Hata hivyo, baadhi yao hawakupata alama zote kwa sababu walichanganya na maelezo yanayoweza kumsaidia mtumiaji kuepuka ajali kwa kutumia alama zilizo barabarani. Kwa mfano, baadhi ya watahiniwa walieleza: *waenda kwa miguu kuzingatia alama za barabarani wakati wa kuvuka barabara*. Kielelezo Na.15 kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu swali hili kwa usahihi.

15. Alama za barabarani Ni maandishi/michoro
inayotumika na watumiaji wote wa barabara katika
kutoa taarifa, maelekezo pamoja na hatari. alama
hizi zinaweza kuwa michoro au maandishi. Zifuatazo
ni njia zitumikazo katika kuepuka ajili zinazosaba
bishwa na ukosefu wa alama za barabarani :-
Kutoa elimu kwa watumiaji wa barabara; Wapo
watumiaji wengi sana wa barabara walembea kwa
miguu na wanaotumia vyombo vya moto barabarani sasa
ili kuepusha ajali wanapaswa kuelimishwa juu ya matu
mizi sahihi ya barabara kwa makundi yote hayo yana
yotumia barabara mfano madereva wa vyombo vya moto
na watu wanaopita kwa miguu katika barabara hiyo
itasaidia kuepusha ajali za barabarani.
Kuweka sheria zitakazoambatana na adhabu kwa
watumiaji wa barabara; Ajali zitaweza kuepukika
kutokana na kuweka sheria kali kwa wanaoendesha
vyombo vya moto na kuweka adhabu kwa kila ataka
evunja sheria hizo za barabarani mfano wa adhabu
ni kufungwa, na kuandikiwa faini kubwa kama
fundisho ili watu wengine wasivunje sheria hizo
za barabarani.
Kuwa makini kwa watembeaji wa miguu pindi
wanapokuwa barabarani: Watu wanaotembea barabarani
wanapaswa kuwa makini katika utembeaji wao
au uvukaji wa barabara watu wengi hawawi
makini katika kuvuka barabara au wanapotembe
a barabarani hiyo inapelekea mtu kupata ajali bila
kutegemea ili kuepuka ni kuwa makini wakati
wa kutembea au kuvuka barabara.

15. Vyombo vya moto kufanyiwa marekebisho kila
mara; Ajali nyingi husababishwa na vyombo
vya moto kutofanyiwa marekebisho ya kila mara
mfano breki za magari zinapaswa kukaguliwa kila
mara ili kuepuka kupata ajali gari linapokosa breki
linaweza kusababisha ajali kubwa sana hivyo ni
vizuri kuchunguzwa kwa magari na kufanyiwa matenge
nezo ya kila mara.
Kuweka matuta katika sehemu za makazi ya
watu ili kupunguza magari yaendayo kasi; katika maene
o ya makazi ya watu panatakiwa kuwekwa matuta
katika barabara ili magari yaweze kupunguza mwe
ndo yanapo karibia eneo hilo pasipo kuwa na
matuta inapelekea watu wengi kupata ajali kwasaba
bu ya magari yaendayo kwa kasi.
Hivyo Ajali zina madhara makubwa mno
mtu anaweza kupoteza, maisha, pia mtu anaweza
kupata kilema cha maisha hivyo ni vyema kuchu
kua tahadhari kwa wakati wa utumiaji wa barabara.


Kielelezo Na. 15: Sampuli ya jibu ambalo siyo sahihi katika swali la 15.

Kielelezo Na.15 kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu swali hili kwa usahihi.

Kwa upande mwingine, watahiniwa (46.3%) waliofaulu kwa kiwango cha wastani walieleza kwa kina hoja mbili au tatu za namna ya kuepuka ajali lakini walichanganya na hoja za kuepuka ajali zinazosababishwa na kutokufuata alama za barabarani. Baadhi yao walitoa hoja zinazoendana na swali lakini maelezo yao hayakutosheleza matakwa ya swali. Aidha, watahiniwa waliopata kiwango hafifu cha ufaulu kuanzia alama 0 hadi 5.5 walishindwa kuelewa matakwa ya swali kwani baadhi yao walieleza jinsi ya kuepuka ajali kwa kutumia alama za barabarani. Wengine walieleza utangulizi na kisha madhara yanayotokana na ukosefu wa alama muhimu za barabarani. Kwa mfano mmoja wa watahiniwa aliandika: *Ukosefu wa alama muhimu barabarani unaweza kusababisha vifo au ulemavu wa kudumu unaosababishwa na ajali.*

### 2.2.6 Swali la 16: Ufundishaji wa Mada za Mfano


Katika swali hili watahiniwa walitakiwa kuchanganua hatua tano muhimu zinazofanywa na shirika la posta ili barua iweze kumfikia anayetumiwa. Swali hili ni miongoni mwa maswali ambayo hayakuwa ya lazima. Watahiniwa 852 (23.0%) walijibu swali hili, kati yao watahiniwa 51 (6.0%) walipata alama kuanzia 10.5 hadi 15. Takwimu zinaonesha kuwa watahiniwa 181 sawa na asilimia 21.2 walipata alama kuanzia 6 hadi 10.0 na watahiniwa 620 sawa na asilimia 72.8 walipata alama 0 hadi 5.5. Chati Na.10 inaonesha ufaulu wa watahiniwa katika swali hili.




**Chati Na. 10:** *Ufaulu kwa watahiniwa katika swali la 16.*

Kwa ujumla, swali hili lilikuwa na kiwango hafifu cha ufaulu kwa sababu asilimia 72.8 ya watahiniwa walipata chini ya alama 5.5 kama inavyooneshwa katika Chati Na.10. Kiwango hiki hafifu cha ufaulu kimesababishwa na watu wengi kwenye jamii kutokutumia shirika la posta kutuma barua badala yake njia za mawasiliano kama simu na barua pepe zinatumiwa kwa sasa. Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa, baadhi ya watahiniwa waliopata alama 0 hadi 1.5 walieleza hatua muhimu zinazofanywa na mtumaji wa barua kwa njia ya posta badala ya hatua zinazofanywa na shirika la posta ili barua iweze kumfikia anayetumiwa. Kwa mfano, baadhi ya watahiniwa waliandika: *Kuweka barua kwenye bahasha, kufunga bahasha, kubandika stempu na kuweka kwenye sanduku la Posta.* Aidha, watahiniwa wengine waliandika utangulizi na hatua moja tu sahihi (kusafirisha barua) lakini walishindwa

kueleza hatua zingine. Kielelezo Na.16.1 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa ambaye hakujibu kwa usahihi.


16. Shirika la Posta ni shirika ambalo huhusika
na usafirishaji wa barua, fedha kwa njia ya mtandao
Shirika la Posta huhusika na kutuma na kupokea
barua, kutuma hawala za fedha, kutuma vifurushi
Shirika la posta linaweza kuwa shirika la ndani
ya nchi na huweza kutuma kwenda nje ya nchi.
Zifuatazo ni hatua muhimu zinazofanywa na shirika
la posta ili barua iweze kufika kwa anayetumiwa
Hatua ya kwanza ni kuandaa barua yako na
kisha kuikunja vizuri. katika hatua hii barua huwe
za kukunjwa na kisha kuwekwa kwenye bahasha
uliyoiandaa ili uweze kuitumia kwa mtu unaye
ta kumfikia wakati uhitaji unafika kumtumia.
Mfano utakunja barua yako kisha na kuiweka
kwenye bahasha yako utakayotuma.
Hatua ya pili ni kubandika stempu juu
ya bahasha kwa upande wa kulia. katika hatua hii
huweza kubandikwa stempu na stempu hiyo ina
yobandikwa ni muhimu kuzingatia uzito ili ien
dane na gharama yako utakayotumia kutumia
barua yako kwenda mahali panapotakiwa kwa
wakati huo, kwasababu stempu huendana na
gharama ya kutuma kwa mpokeaji anayemtumi
a barua uliyoiandika wakati huo.
Hatua ya tatu ni kuandika jina lake kwa
usahihi. Barua huwa upande wa kuingiza kwenye
bahasha ni muhimu kuandikwa anwani ya
mpokeaji wa mtu ambaye ataipokea kwenye
posta yake ni muhimu aandikiwe jina kwa
usahihi ili wakati wa kutafuta siwe shida
kuipata barua yako wakati huo anapokea.

Kielelezo Na 16: Sampuli ya jibu lisilo sahihi kwa swali la 16.

Kielelezo Na. 16 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyeonesha uelewa wa shirika la posta katika utangulizi lakini alishindwa kuchanganua hatua muhimu zinazotumiwa na shirika hilo kufikisha barua kwa mhusika.

Pamoja na swali hili kuwa na kiwango hafifu cha ufaulu, watahiniwa 181 (21.2%) walifaulu kwa kiwango cha wastani. Baadhi ya watahiniwa hawa walichanganua hatua sahihi mbili kwa usahihi au tatu kati ya hatua tano zilizotakiwa. Uchambuzi ulionesha pia kwamba, watahiniwa wengine walitaja hatua zinazofanywa na shirika la posta katika kusafiririsha barua bila maelezo yanayojitosheleza. Mwisho watahiniwa wengine walichanganya hatua zinazotumiwa na shirika la posta kusafirisha barua kumfikia mhusika na hatua za kuandaa barua ili iweze kusafirishwa kwa njia ya posta.

Asilimia 6 tu ya watahiniwa walifaulu kwa kiwango kizuri. Baadhi yao, walikua na uelewa uliowawezesha kuchanganua kwa usahihi hatua tano muhimu zinazofanywa na shirika la posta ili barua iweze kumfikia mlengwa. Hatua zilizochanganuliwa na watahini ni pamoja na: *kukusanya barua, kugonga mihuri, kupanga katika mafungu kulingana na mahali zinapoenda, kusafirisha barua na kuweka katika boksi la sanduku husika la posta*. Hata hivyo, baadhi yao walishindwa kupata alama zote kwa sababu hawakuchanganua hatua ya pili ambayo ni kupanga barua katika mafungu kulingana na mahali zinapoenda.

## 3.0 UCHAMBUZI WA KIWANGO CHA UFAULU KATIKA MADA

Uchambuzi wa kiwango cha ufaulu kwa watahiniwa unaonesha kuwa somo la TEHAMA 2020 lilikuwa na kiwango kizuri cha ufaulu. Uchambuzi zaidi uliofanyika katika mada unaonesha kuwa, watahiniwa walikuwa na kiwango kizuri cha ufaulu katika mada 3. Mada hizo ni: *Maandalizi ya Ufundishaji na Ujifunzaji wa Somo la TEHAMA (87.4%), Misingi ya Ufundishaji na Ujifunzaji wa Somo la TEHAMA (83.2%) na Upimaji (82.9%)*. Kiwango kizuri cha ufaulu katika mada hizi huenda kilisababishwa na watahiniwa kutumia zana katika ufundishaji na ujifunzaji wa somo la TEHAMA, kutumia misingi ya ufundishaji na ujifunzaji wa somo la TEHAMA katika ujifunzaji na ufundishaji. Sababu nyingine ni kufanya kazi mradi katika kuandaa mazoezi, kusahihisha na kuandaa maswali mbalimbali.

Aidha, mada moja ya *Ufundishaji wa Mada za Mfano* ilikuwa na kiwango cha ufaulu cha wastani (49.4%). Kiwango hiki cha ufaulu cha wastani katika mada hii kinaweza kuwa kilisababishwa na watahiniwa kutofanya ziara mafunzo katika maktaba na kutofanya kazi mradi katika kutafuta maandiko mbalimbali katika maktaba.

## 4.0 HITIMISHO

Kwa ujumla kiwango cha ufaulu cha watahiniwa kilikuwa kizuri kwa sababu asilimia 99.9 ya watahiniwa wote waliofanya mtihani huu walifaulu. Watahiniwa walijibu maswali mengi kwa usahihi jambo linalodhihirisha kuwa, walikuwa na maarifa ya kutosha katika mada zilizotahiniwa.

Hata hivyo, pamoja na kiwango cha ufaulu kuwa kizuri, baadhi ya watahiniwa walifanya makosa wakati wa kujibu baadhi ya maswali kutokana na ama kutoelewa matakwa ya maswali au kukosa maarifa ya kutosha kwenye dhana zilizotahiniwa.

Tathmini ya uchambuzi kwa kila swali ilionesha kuwa, watahiniwa walipata kiwango kizuri cha ufaulu katika swali la 6 na 7 yaliyotoka katika mada ya *Maandalizi ya Ufundishaji na Ujifunzaji wa Somo la TEHAMA*. Maswali mengine yaliyokuwa na kiwango kizuri cha ufaulu ni swali la 4 na 13 yaliyotungwa kutoka kwenye mada ya *Upimaji*. Vilevile, swali la 1, 11 na 14 yaliyotungwa kwenye mada ya *Misingi ya Ufundishaji na Ujifunzaji wa Somo la TEHAMA* yalikuwa na kiwango kizuri cha ufaulu. Maswali mengine ambayo watahiniwa walifaulu kwa kiwango kizuri ni swali la 5, 12 na 15 yaliyotoka kwenye mada ya *Ufundishaji wa Mada za Mfano*.

Uchambuzi zaidi unaonesha kuwa, watahiniwa walifaulu kwa kiwango hafifu katika swali la 3, 8, 10 na 16 yaliyotoka kwenye mada ya *Ufundishaji wa Mada za Mfano* (Angalia Kiambatisho).

## 5.0 MAPENDEKEZO

Ili kuboresha zaidi kiwango cha ufaulu cha watahiniwa katika somo la TEHAMA mambo yafuatayo yanapendekezwa:

(a) Wakufunzi waandae ziara mafunzo katika maktaba za aina mbalimbali ili walimu tarajali waweze kujifunza na kuona mpangilio wa maandiko katika maktaba. Aidha, wafanye ziara mafunzo kuona alama za barabarani na matumizi yake katika mawasiliano.

(b) Wakufunzi waandae maswali na majibu yatakayowaongoza walimu tarajali kujifunza kwa mfano (demonstration) matumizi ya huduma ya posta na kusoma vijarida mbalimbali vinavyohusu, kutuma na kupokea barua, vifurushi, hawala ya fedha na rejista.

*Kiambatisho*

**MUHTASARI WA UFAULU WA WATAHINIWA KATIKA SOMO LA TEHAMA**

<table>
<tr><th>Na.</th><th>Mada</th><th>Na. ya swali</th><th>Ufaulu Katika Kila Swali (%)</th><th>Wastani wa Ufaulu Katika Kila Mada (%)</th><th>Maoni</th></tr>
<tr><td rowspan="2">1.</td><td rowspan="2">Maandalizi ya Ufundishaji na Ujifunzaji wa Somo la TEHAMA</td><td>6</td><td>75.1</td><td rowspan="2">87.4</td><td rowspan="2">Vizuri</td></tr>
<tr><td>7</td><td>99.6</td></tr>
<tr><td rowspan="3">2.</td><td rowspan="3">Misingi ya Ufundishaji na Ujifunzaji wa Somo la TEHAMA</td><td>14</td><td>95.4</td><td rowspan="3">83.2</td><td rowspan="3">Vizuri</td></tr>
<tr><td>1</td><td>81.7</td></tr>
<tr><td>11</td><td>72.4</td></tr>
<tr><td rowspan="3">3.</td><td rowspan="3">Upimaji</td><td>2</td><td>61.4</td><td rowspan="3">82.9</td><td rowspan="3">Vizuri</td></tr>
<tr><td>13</td><td>88.0</td></tr>
<tr><td>4</td><td>99.3</td></tr>
<tr><td rowspan="8">4.</td><td rowspan="8">Ufundishaji wa Mada za Mfano</td><td>8</td><td>1.1</td><td rowspan="8">49.4</td><td rowspan="8">Wastani</td></tr>
<tr><td>10</td><td>17.3</td></tr>
<tr><td>3</td><td>27.5</td></tr>
<tr><td>16</td><td>27.2</td></tr>
<tr><td>9</td><td>40.0</td></tr>
<tr><td>12</td><td>85.6</td></tr>
<tr><td>15</td><td>97.2</td></tr>
<tr><td>5</td><td>99.1</td></tr>
</table>